SautiElimu

Toleo la 9
2005
ISSN 1821 - 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Ni haki yako kuuliza maswali, kutoa maoni

Na Rakesh Rajani, Mkurugenzi Mtendaji, HakiElimu

Katiba ya nchi yetu inasema " Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba...Serikali itawajibika kwa wananchi..."

Wazo la kuwa na *Marafiki wa Elimu* msingi wake ni kwa wananchi wenyewe, kama watendaji wakuu, kushiriki kuleta mabadiliko wao wenyewe na pia kuiwajibisha Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Habari zilizochapishwa katika jarida hili zinaonyesha wazi matendo ya wananchi katika kuleta mabadiliko. Mathalan; Wananchi wa Musoma walileta mabadiliko kwa kuhoji matumizi ya fedha za MMEM, Arusha wana mkakati wa kuwapa motisha walimu na Ukonga wameanza utaratibu wa kuhakiki ubora wa majengo ya shule.

Inaelekea kuwa wazo la wananchi kufanya vitendo vya kuleta mabadiliko linapata upinzani katika baadhi ya sehemu nchini. Unaweza kuulizwa "Unafanya hivyo kama nani?" au "Kwani wewe nani?" Jibu ni kwamba; "Mimi ni mwananchi mwenye haki kwa mujibu wa Katiba". Tunahitaji kujenga utamaduni Tanzania ambapo wananchi wa kawaida watajisikia huru kuuliza maswali, kutoa mawazo yao na kushiriki kwa vitendo katika kuleta mabadiliko.

Harakati za Marafiki wa Elimu Tanzania ni za watu ambao wameshaanza kutekeleza haki yao ya kikatiba. HakiElimu ni mraghabishi wa harakati hizo. *Marafiki* si mawakala wala wawakilishi wa HakiElimu. Hawafanyi kazi wala hawapokei mwongozo kutoka HakiElimu. Hawasubiri kuambiwa nini cha kufanya. Marafiki wenyewe, kama watu binafsi au vikundi, wanaamua cha kufanya – kwa mujibu wa sheria – kuifanya elimu na demokrasia kuwa hai katika jumuiya zao. Utajiunga nao?

Marafiki wa Elimu mnafanya nini?

Na Walter de Nijs, Babati-Arusha

Nasikitika kuona *Marafiki wa Elimu* wengi wanaoliandikia jarida hili wanatoa ushauri tu kwa watu wengine bila kueleza wao wanafanya nini. Naomba fursa na kuelezea sisi *Marafiki* wa Babati tunafanya nini kuboresha elimu ili kutoa changamoto kwa wengine.

Kupitia shirika letu la Local Initiatives Support Organisation (LISO), tumechagua maeneo ya kushughulikia katika harakati za kuboresha elimu. Kwanza, kuna majengo ya madarasa yenye madirisha madogo yasiyopitisha mwanga. Pili, kuna uhaba wa vifaa vya kufundishia, vikiwemo vitabu vya ziada pia nyumba za walimu hazitoshi.

Marafiki wameandaa mikakati ya kuwapa motisha walimu na wanafunzi. Kwa upande wa walimu, hivi karibuni, kamati ya shule iliandaa sherehe ya kuwapongeza walimu (bila walimu kujua). Hii iliwapa moyo sana walimu ambao walijisikia kuwa kweli wazazi wanawajali. Tukumbuke kuwa mwalimu ambaye hana raha kazini atapata shida sana kufundisha watoto.

Upo utaratibu pia wa kuwapa motisha watoto ili waache utoro na kupenda kuja shuleni. Tunatafuta wafadhili wa kutusaidia kununua vifaa vya michezo na jezi kwa ajili ya wanafunzi. Vilevile tunatafuta vyombo vya muziki/bendi. Hatua hii tunaamini itawavutia watoto kuja shuleni na kuacha utoro.

Ningependa kupata taarifa na uzoefu kutoka kwa wadau wengine. Wanafanya nini? Wanajifunza nini? Wanahusisha vipi watoto wenye ulemavu? Wanawasaidia vipi watoto masikini ambao wanashindwa kwenda shule kwa kukosa sare au mahitaji mengine muhimu? Wanafanya nini kuhamasisha wazazi kushiriki katika kuboresha elimu?

Marafiki wapania kuboresha elimu

Na Mary Nsemwa, Idara ya Ushiriki Mwananchi, HakiElimu

Tarehe 10 Machi mwaka huu, *Marafiki wa Elimu* walikutana jijini Dar es Salaam kujadili ushiriki, wajibu, majukumu, mategemeo na umiliki wa Harakati za *Marafiki wa Elimu.*

Katika mkutano huo, *Marafiki* walijadili uelewa wao juu ya harakati hizi, mafanikio waliyoyapata na changamoto zinazowakabili. Baadhi ya mafanikio ya kazi za *Marafiki* ni kuweza kuhamasisha na kushawishi jamii kufahamu na kujadili mafanikio na matatizo ya sekta ya elimu nchini.

Baadhi wameweza kuwashawishi wazazi kupeleka watoto wao shule. Kwa mujibu wa washiriki, mijadala katika jamii imefanikiwa kutokana na mwongozo mzuri wa Serikali unaotoa uhuru wa kuhoji, kuuliza maswali na kujadili sera mbalimbali zinazowagusa wananchi. *Marafiki* pia wametoa changamoto kwa watu kusoma machapisho yaliyoandikwa kwa lugha rahisi kuhusu sera mbalimbali, yanayosambazwa na HakiElimu.

Marafiki walizitaja changamoto kuwa ni jamii kutotenga muda wa kutosha kujadili masuala muhimu ya elimu. Nyingine ni wazazi kutofahamu sera na miongozo kuhusu ushiriki hasa wa wanafunzi katika kamati za shule.

Marafiki wengi wanashindwa kutofautisha kati ya *Harakati za Marafiki wa Elimu* na HakiElimu. Wengine hudhani kuwa HakiElimu ni moja kati ya idara za Serikali. *Marafiki* pia hukwama wanapowahoji baadhi ya watendaji wanaopindisha utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali.

Marafiki hukutana na maswali kama "wewe unauliza kama nani?" Wakati mwingine hudaiwa vitambulisho vinavyowapa mamlaka ya kufuatilia na kuuliza maswali! Hii inaonyesha kuwa haki ya kikatiba ya mwananchi kuzungumza na kutoa mawazo yake bado haieleweki sehemu nyingi nchini.

Baadhi ya *Marafiki* hawafahamu nini kifanyike kumsaidia *Rafiki wa Elimu* akipata matatizo na wengine hawajui wajibu wao.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, washiriki walipendekeza kujenga mitandao madhubuti miongoni mwa *Marafiki* ili kubadilishana mawazo, uzoefu na habari za elimu. Nyingine ni kuwajibika katika harakati za kuboresha elimu, kuhimiza wazazi kushiriki na kufuatilia maendeleo ya watoto shuleni. Wamependekeza pia kutumia mitandao mbalimbali ya mawasiliano ili kusaidiana wakati wanapopata matatizo. Mathalan kutumia vyombo vya sheria na habari, tovuti na barua.

Musoma wahoji matumizi pesa za MMEM

***Marafiki wa Elimu*, SLP 1252, Majita- Musoma**

Wananchi wa Majita, Musoma wameitaka kamati ya shule kusoma taarifa halisi ya mapato na matumizi ya fedha za shule katika mkutano wa wazazi.

Hatua hiyo ilifikiwa na wananchi baada ya kusoma miongozo mbalimbali ya Serikali na kugundua kwamba wana haki ya kuhoji matumizi ya fedha za shule. Miongozo hiyo ilitumwa na HakiElimu kwa *Marafiki wa Elimu* wa eneo hilo.

Baada ya kuyasoma machapisho na kupata mwanga, wazazi na *Marafiki*, kupitia serikali ya kijiji waliomba uitishwe mkutano wa hadhara. Katika mkutano huo wazazi walidai haki yao ya kusomewa taarifa na hasa za ruzuku kwa kila mwanafunzi (Capitation Grant).

Wakati wa kusomewa mahesabu, wananchi waligundua kwamba baadhi ya taarifa za fedha hazikulingana na matumizi na nyingine hazikuwa sahihi. Walishauri Mratibu Elimu Kata apeleke taarifa katika ngazi ya juu ili kuizuia kamati ya shule hiyo isitoe fedha benki mpaka itakapotoa taarifa sahihi za mapato na matumizi ya fedha za shule.

Mkutano huo wa wazazi pia ulitoa mapendekezo kwa Ofisi ya Ukaguzi kuzitembelea shule mara kwa mara na kukagua matumizi ya fedha za MMEM.

Wananchi walishauri *Marafiki* wengine kote nchini kushirikiana na Serikali katika kutekeleza mipango ya maendeleo. Moja ya majukumu ya *Marafiki wa Elimu* ni kuchangia kwa mawazo na vitendo harakati za kuboresha elimu.

Baadhi ya fedha za MMEM ni mkopo kwa Serikali ambapo kila mwananchi atawajibika kulipia kwa njia ya kodi. Fedha hizo zisipotumika kwa malengo yaliyokusudiwa kwa sasa, watakaoathirika ni watu masikini ambao watabebeshwa mzigo wa kulipia karo za watoto na kununua vitabu!

Ukurasa wa 1

SautiElimu

hakielimu

Toleo la 9
2005
ISSN 1821 - 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Marafiki wa Ukonga wahakikisha vyoo vya shule vinafaa!

***Marafiki wa Elimu*, Ukonga, Dar es Salaam**

Katika harakati za kuleta mabadiliko ya elimu, *Marafiki* wa Ukonga wamehoji gharama halisi zilizotumika kujenga vyoo vya shule.

Hayo yalifanyika katika mkutano wa hadhara wa wazazi kwenye shule moja ya msingi, kata ya Ukonga, jijini Dar es Salaam. Pamoja na gharama za ujenzi, mkutano huo ulijadili ubora wa vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa fedha za MMEM.

Awali *Marafiki* waliotembelea shule hiyo waliona kuwa vyoo vilivyojengwa havikuwa na hadhi, havikujengwa kitaalamu na havikuwa na viwango vya ubora. Vilijengwa kwa matofali mabovu na yasiyofaa. Mkutano huo uliitaka kamati ya shule kutoa hesabu za gharama halisi zilizotumika kujenga vyoo hivyo.

Baada ya kushindwa kutoa maelezo sahihi, serikali ya kijiji iliipa kamati ya shule siku 14 kufanya marekebisho ya hesabu na kukarabati vyoo ili viwe na ubora unaostahili. Huu ni mfano bora wa namna ambayo *Marafiki* wanaweza kuleta mabadiliko na uwajibikaji kwa kushirikiana na Serikali. Je, Marafiki wenzetu popote mlipo, mmeleta mabadiliko gani?

Marafiki wasaidia ongezeko la walimu, wanafunzi kufaulu

Na Petro M. Mgunda, SLP 482, Njombe

Napenda kuwafahamisha *Marafiki wa Elimu* kote nchini mambo ambayo tayari yamefanywa na wenzao huku Njombe.

Kwa kushirikiana na kamati ya shule na Mratibu Elimu Kata, tulikaa kikao na kupeleka maombi yetu kuhusu kuongezewa walimu wilayani. Ushirikiano wetu na viongozi umewezesha kupatikana kwa walimu wa kutosha katika shule nyingi wilayani hapa.

Tumejiwekea mikakati ya kuhakikisha kwamba kila mtoto anayestahili kwenda shule anaandikishwa. Kama *Marafiki*, tunafuatilia na kuhakikisha kila mzazi anatekeleza wajibu wake. Tunayo pia mipango ya kumwajibisha mzazi /mlezi atakayemzuia mtoto wake kwenda shule.

Matunda mengine kutokana na ushirikiano mkubwa kati ya walimu, wazazi na wanaharakati ni kuwezesha kufaulu kwa kiwango cha juu katika shule yetu. Vilevile tumechangia kuwepo kwa vitendea kazi shuleni, majengo, vyoo na viwanja vya michezo.

Tumeshirikiana pia na uongozi wa shule na kamati ya shule kuhakikisha fedha zote zilizotolewa katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) pamoja na michango ya hiari ya wananchi, zinatumika kulingana na mipango iliyokusudiwa.

Tunashauri Marafiki wengine kote nchini waanze kuleta mabadiliko ya elimu kwa vitendo katika maeneo yao.

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari, kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu, uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Shukrani kwa Shule ya Msingi St. Joseph, *Marafiki* wa Songea na Sylvand Jeremiah kwa picha. Shukrani nyingi pia kwa *Marafiki wa Elimu* kote nchini kwa kuchangia kutoa maoni na kuandika habari katika jarida hili.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili kwa HakiElimu.

Mhariri Mkuu: Rakesh Rajani
Mratibu *SautiElimu*: Lilian R. Kallaghe

Tuandikie!

HakiElimu, ***SautiElimu***
SLP 79401
Dar es Salaam
Simu: (022) 2151852 /3
Faksi: (022) 2152449
Baruapepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

ISSN 1821-5076

© HakiElimu, 2005

Barua kwa SautiElimu

‘Nawatembelea nyumba kwa nyumba kuhamasisha uandikishaji shule’

Na Yonafika Dickson, SLP 111, Bulyankulu, Tabora



Nimeamua kutembelea shule na familia mbalimbali hapa kijijini kujadiliana nao na kuwahamasisha juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto. Nimefanya hivyo baada ya kusoma miongozo inayoeleza kuwa kila mtoto ana haki ya kupata elimu.

Wapo baadhi ya wazazi ambao bado wanawazuia watoto wao kwenda shule ili wawasaidie katika miradi yao mbalimbali. Nimetembelea shule 4 hapa Bulyankulu na kuzungumza na wanafunzi ambao wengi wao hawakujua kwamba elimu ni haki yao. Nimewapa mbinu mbalimbali za kuweza kuwasaidia watoto wenzao ambao wananyimwa haki yao ya kupata elimu pamoja na wazazi wao.

Nimefanya pia ziara katika familia 9 ambazo hawakutaka watoto wao wasome. Familia 3 kati ya hizo 9 hazijawahi kwenda shule hata ya chekechea! Kuanzia baba, mama na watoto wote. Sababu kubwa ni umasikini. Wazazi hawana fedha za kuwanunulia watoto sare na vifaa vingine vya shule.

Kwa ujumla, nilifanya majadiliano na familia 23. Matokeo yake, watoto 38 waliandikishwa kuanza darasa la kwanza na wazazi zaidi ya watatu walijiunga na darasa la Elimu ya Watu Wazima.

Kwanini fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi zinachelewa?

Na Mganga Semwija, SLP 21 Kidugalo, Ngerengere-Morogoro

Naipongeza Serikali kwa majengo mazuri ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Hata hivyo, bado yapo matatizo ambayo yanaathiri upatikanaji wa elimu bora.

Baadhi ya matatizo hayo ni ucheleweshaji wa fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi, dola 10 (Capitation Grant). Fedha hizi zinatumwa kwa mafungu na hazifiki kwa wakati mwafaka. Tatizo lingine ni upungufu wa walimu. Mathalan, bado ziko shule zenye wanafunzi 500 lakini walimu ni 7 tu. Kwa hali hiyo walimu watawezaje kutoa elimu bora?

Madawati na samani pia bado ni tatizo kubwa. Fedha zilizotolewa hazitoshi kutengeneza madawati ya kutosha. Wananchi wamekuwa wakitoa michango ya hali na mali kukabiliana na tatizo hili lakini michango yao ni kidogo kutokana na ugumu wa maisha.

Maslahi ya walimu bado yana utata. Marekebisho ya mshahara baada ya kupanda daraja hayafanyiki kwa wakati. Fedha za uhamisho hazipatikani kwa wakati ama hazipatikani kabisa! Hali hii inasababisha walimu kukata tamaa na kujiingiza katika shughuli binafsi badala ya kufundisha.

Matatizo niliyoyataja, kama hayatafanyiwa kazi mara moja, tutaishia kuwa na majengo mazuri bila elimu bora.

MMEM isiishie 2006 !

Na Michael Magoma, SLP 113, Shinyanga

Wakati MMEM inaelekea ukingoni mwaka ujao (2006) nashauri Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kuwa fedha zilizotolewa kote nchini zimetumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Nashauri hivyo kwa sababu kuna uwezekano shule zingine zikaachwa zikiwa katika hali duni kutokana na uzembe wa baadhi ya viongozi. Huenda fedha zinatolewa kwa wakati Wizara ya Fedha lakini hazifuatiliwi kwa makini kuona kama zinafika shuleni kwa wakati.

Mambo ya kufuatilia ni: Je, kila shule ina vifaa vya kufundishia, vyumba vya madarasa na vyoo vya kutosha? Nyumba za walimu je? Maji na mazingira ya shule yanaridhisha?

Napendekeza pia yawepo maandalizi ambayo yatawezesha MMEM kuwa endelevu. Hii itasaidia sio tu shule ambazo zitakuwa hazijakamilisha mipango yake bali pia kuongeza kiwango cha ubora wa elimu.

Fedha za mafunzo kwa walimu zinatumikaje?

Na M. Ngurangwa, SLP 193, Masasi-Mtwara

Juhudi za kuboresha elimu zinakwamishwa na baadhi ya watendaji wa Serikali wilayani. Utakuta sera inasema walimu wapate mafunzo kila baada ya mufa fulani ili kuongeza ujuzi na kwenda na wakati.

Walimu wengi wanapenda kujiendeleza na elimu ya juu ya diploma lakini wanapata upinzani kutoka kwa baadhi ya watendaji wa wilaya na halmashauri.

Wanawawekea walimu vikwazo na kukataa kuwalipia kozi bila sababu za msingi. Ikiwa Serikali inahimiza walimu wajiendeleze lakini wakati huohuo watendaji wake wanaweka vikwazo, tufanyeje? Kwa nini Halmashauri ambazo zinakaa muda mrefu bila kupeleka walimu kwenye mafunzo hazichukuliwi hatua?

Nashauri Serikali ifuatilie kwenye halmashauri kote nchini kujua jinsi fedha za mafunzo ya walimu zilivyotumika.

Ukurasa wa 2